



## EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

### **MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MAFUTA KWA MAGARI NA VIFAA VINGINE KWENYE MAENEO YA MKUZA WA BOMBA LA MRADI WA EACOP. KUMBUKUMBU Na. 0010007537**

Kampuni ya EACOP LTD ya nchini Tanzania Inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya kutoa huduma za mafuta kwa ajili ya magari na vifaa vingine katika maeneo ya mkuza wa bomba la mafuta katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443 kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

#### **MAELEZO MAFUPI YA MRADI**

- Mwombaji awe amekidhi vigezo vya Sheria ya OSHA ya Tanzania ya mwaka 2003, pamoja na kuambatanisha na Cheti cha OSHA.
- Kukidhi kiwango cha chini cha mahitaji ya kituo cha mafuta kwa mujibu wa Sheria ya EVVURA sura ya 414, na Sheria ya mafuta ya Petroli sura ya 392, ya mwaka 2015 au kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.
- Kuzingatia utunzaji wa mazingira.
- Awe amethibitishwa na kukidhi vigezo vya udhibiti wa majanga ya moto.
- Kuzingatia viwango vya TBS TZS 672: 2012 - EAS 158:2012 ICS 75.160,20; TZS 674: 2012 - EAS 177:2012 ICS 75.160.20; TZS 1076:2008 TZS 1115: 2009.
- Vituo vya mafuta viwe katika maeneo yafuatayo, Muheza, Handeni, Wilaya Kilindi, Kibirashi, Kiteto (Kibaya), Hanang, Chemba, Igunga, Kagongwa, Bukombe (Ushiroambo), Chato, Muleba, Misenyi (Mutukula), Kyaka.
- Kituo cha mafuta au kampuni zinazoweza kutoa kwa wateja kadi za kununua mafuta zenye miraba ya sumaku, au misimbo ya kufungulia na nambari ya utambulisho ya siri au nambari ya usalama) zitapewa kipaumbele.

#### **VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kusajiliwa kama muuzaji wa mafuta/ Kituo cha mafuta/Kampuni ya mafuta kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Leseni ya kufanya kazi kutoka Tume ya Kudhibiti Nishati.
- Maelezo mafupi ya uzoefu katika huduma za kukodisha na matengenezo ya gari.
- Taarifa ya uzoefu inayoonyesha angalau shughuli tatu (3) zinazofanana hizi.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa ya fedha ya mwaka.
- Wakati wa kuwasilisha majibu ya kuonesha nia, waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Ushahidi wa taasisi kuhusu usimamizi wa mfumo na sera za HSE, utaratibu na mchakato kwa kuzingatia viwango vya ndani na Viwandani vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hizi.
- Leseni stahiki kutoka kwa mamlaka husika za ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma.
- Orodha ya wateja watano (5) bora ikijumuisha huduma zitolewazo kwa wateja.
- Cheti cha Usajili (ambatisha nakala).
- Wasifu wa mtu atakayehusika na mawasiliano na upande wa Mradi.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma maombi ya kuonyesha nia yao pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya [eacop-tz.eoi.100001@totalenergies.com](mailto:eacop-tz.eoi.100001@totalenergies.com) (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tare **29 machi 2022** saa **11 : 00** jioni saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kinapaswa kuwa ni **0010007537**.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. **Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho.** Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonyesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza .